wa Usafirishaji wa Meli na Mizigo, Usimamizi wa Usafiri na Mnyororo wa Ugavi, Ubunifu wa Meli na Uhandisi wa Bahari ya Nje (Offshore Engineering).

#### 6.1.4 Uhandisi wa Nishati, Madini na Sayansi ya Ardhi

Uhandisi wa Nishati Jadidifu (Umeme wa Maji, Upepo, Jua), Uhandisi wa Mabomba, Mafuta na Gesi, Teknolojia ya Uhandisi wa Mafuta na Gesi, Uhandisi na Usimamizi wa Mazingira, Utengenezaji wa Vito na Mapambo, Uchimbaji na Uchakataji wa Madini, Jiolojia na Utafiti wa Madini, Jiolojia ya Mafuta na Utafiti, Upimaji wa Ardhi na Migodi, Uhandisi wa Metallojia na Uchakataji wa Madini, na Uhandisi wa Migodi.

#### 6.1.5 Kilimo na Mifugo

Teknolojia ya Ngozi, Teknolojia ya Chakula na Lishe ya Binadamu, Teknolojia ya Uzalishaji wa Sukari, Teknolojia ya Kilimo cha Miwa, Teknolojia ya Maabara ya Mifugo, Kilimo cha Bustani, Uhandisi wa Umwagiliaji na Uchepuaji wa Kilimo (Agro Mechanization).

## 6.2 Programu za Mkupuo wa Pili (Cluster Two)

Mkupuo huu unajumuisha wanafunzi waliodahiliwa katika fani zifuatazo; Uhandisi wa Nishati, Madini na Sayansi ya Ardhi, TEHAMA (ICT), pamoja na Kilimo na Mifugo ambazo hazikutajwa katika kifungu cha **6.1.4** na **6.1.5.** Wanafunzi wa fani hizi wanastahili kuomba mkopo.

## 6.3 Orodha ya Programu za Stashahada Zenye Sifa ya Kupata Mkopo

### 6.3.1 Afya na Sayansi Shirikishi

(i) Stashahada ya Udaktari wa Meno,
(ii) Stashahada ya Mionzi ya Utambuzi wa Magonjwa,
(iii) Stashahada ya Tiba ya Kazi,
(iv) Stashahada ya Tiba ya Viungo (Physiotherapy),
(v) Stashahada ya Uhandisi wa Umeme na Vifaa vya Tiba (Biomedical),
(vi) Stashahada ya Sayansi ya Afya ya Mazingira,
(vii) Stashahada ya Teknolojia ya Taarifa za Kumbukumbu za Afya,
(viii) Stashahada ya Sayansi ya Maabara ya Tiba,
(ix) Stashahada ya Utambuzi wa Magonjwa kwa kutumia Macho (Clinical Optometry),
(x) Stashahada ya Lishe ya Tiba (Clinical Nutrition), na
(xi) Stashahada ya Juu ya Uuguzi wa Afya ya Akili.

### 6.3.2 Usafirishaji na Usimamizi wa Mizigo

(i) Stashahada ya Ufundi wa Ndege,
(ii) Stashahada ya Ujenzi na Ukarabati wa Meli,
(iii) Stashahada ya Ujenzi na Matengenezo ya Reli,
(iv) Stashahada ya Usafirishaji wa Kimataifa na Usimamizi wa Mnyororo wa Ugavi,
(v) Stashahada ya Usafiri wa Baharini na Sayansi ya Ubaharia,
(vi) Stashahada ya Usimamizi wa Usafirishaji wa Meli na Mizigo,

(vii) Stashahada ya Usimamizi wa Usafiri na Mnyororo wa Ugavi,
(viii) Stashahada ya Ubunifu wa Meli na Uhandisi wa Nje ya Bahari,
(ix) Stashahada ya Uhandisi wa Mitambo na Uhandisi wa Bandari,
(x) Stashahada ya Uhandisi wa Treni za Dizeli na Umeme,
(xi) Stashahada ya Usimamizi wa Usafirishaji wa Meli na Bandari,
(xii) Stashahada ya Uhandisi wa Baharini, na
(xiii) Stashahada ya Usafirishaji wa Meli na Operesheni za Bandari.

### 6.3.3 Uhandisi wa Nishati, Madini na Sayansi ya Ardhi

(i) Stashahada ya Teknolojia ya Nishati Jadidifu (Umeme wa Maji, Upepo, Jua),
(ii) Stashahada ya Mabomba,
(iii) Stashahada ya Uhandisi wa Mafuta na Gesi,
(iv) Stashahada ya Teknolojia ya Uhandisi wa Mafuta na Gesi,
(v) Stashahada ya Uhandisi wa Mazingira na Usimamizi,
(vi) Stashahada ya Utengenezaji wa Vito na Mapambo,
(vii) Stashahada ya Uchakataji wa Madini,
(viii) Stashahada ya Jiolojia na Utafiti wa Madini,
(ix) Stashahada ya Jiolojia ya Mafuta na Utafiti,
(x) Stashahada ya Upimaji wa Ardhi na Migodi,
(xi) Stashahada ya Uhandisi wa Metallojia na Uchakataji wa Madini,
(xii) Stashahada ya Uhandisi wa Migodi,

(xiii) Stashahada ya Uhandisi wa Umeme na Umeme wa Maji,
(xiv) Stashahada ya Jiolojia ya Maji na Uchimbaji wa Visima,
(xv) Stashahada ya Hydrology na Meteorology,
(xvi) Stashahada ya Uhandisi wa Umeme na Mifumo ya Nishati ya Upepo,
(xvii) Stashahada ya Uhandisi wa Umeme na Mifumo ya Nishati ya Jua,
(xviii) Stashahada ya Uhandisi wa Umeme na Nishati Jadidifu,
(xix) Stashahada ya Uhandisi wa Ujenzi na Umwagiliaji,
(xx) Stashahada ya Uhandisi wa Vifaa vya Tiba,
(xxi) Stashahada ya Bioteknolojia,
(xxii) Stashahada ya Uhandisi wa Uchakataji wa Madini,
(xxiii) Stashahada ya Uhandisi wa Mawasiliano na Uashiriaji wa Reli,
(xxiv) Stashahada ya Usimamizi wa Ardhi, Tathmini na Usajili,
(xxv) Stashahada ya Upimaji na Uchoraji Ramani,
(xxvi) Stashahada ya Uhandisi wa Mitambo na Nishati,
(xxvii) Stashahada ya Uhandisi wa Mitambo kwa Mafuta na Gesi,
(xxviii) Stashahada ya Uendeshaji na Matengenezo ya Mifumo ya Maji,
(xxix) Stashahada ya Jiolojia ya Mafuta,
(xxx) Stashahada ya Uhandisi wa Usambazaji na Usafi wa Maji,

(xxxi) Stashahada ya Uhandisi wa Usambazaji wa Maji,
(xxxii) Stashahada ya Upimaji wa Kiasi cha Kazi kwa Maji na Usafi wa Mazingira,
(xxxiii) Stashahada ya Ubora wa Maji na Teknolojia ya Maabara,
(xxxiv) Stashahada ya Mipango ya Miji na Maeneo,
(xxxv) Stashahada ya Uhandisi wa Umeme na Elektroniki,
(xxxvi) Stashahada ya Teknolojia ya Vito na Mapambo,
(xxxvii) Stashahada ya Jiolojia ya Utafiti na Uchimbaji wa Madini,
(xxxviii) Stashahada ya Maendeleo ya Jamii kwa Maji na Usafi,
(xxxix) Stashahada ya Uhandisi wa Umeme, na
(xl) Stashahada ya Uhandisi wa Umeme wa Magari na Elektroniki.

### 6.3.4 Kilimo na Mifugo

(i) Stashahada ya Teknolojia ya Ngozi,
(ii) Stashahada ya Teknolojia ya Chakula na Lishe ya Binadamu,
(iii) Stashahada ya Teknolojia ya Kilimo cha Miwa,
(iv) Stashahada ya Teknolojia ya Uzalishaji wa Sukari,
(v) Stashahada ya Teknolojia ya Maabara ya Mifugo,
(vi) Stashahada ya Kilimo cha Bustani,

(vii) Stashahada ya Uhandisi wa Umwagiliaji na Uchepuaji wa Kilimo,
(viii) Stashahada ya Teknolojia ya Kilimo,
(ix) Stashahada ya Teknolojia ya Mbegu,
(x) Stashahada ya Ubunifu wa Meli na Uhandisi wa Nje ya Bahari,
(xi) Stashahada ya Mipango na Usimamizi wa Matumizi ya Ardhi ya Kilimo,
(xii) Stashahada ya Usimamizi wa Kilimo na Rasilimali Asili,
(xiii) Stashahada ya Uzalishaji wa Kilimo,
(xiv) Stashahada ya Afya ya Wanyama na Uzalishaji,
(xv) Stashahada ya Teknolojia ya Ufugaji wa Samaki,
(xvi) Stashahada ya Uchakataji wa Bidhaa za Maji,
(xvii) Stashahada ya Ufugaji wa Nyuki,
(xviii) Stashahada ya Uzalishaji wa Mazao,
(xix) Stashahada ya Chakula na Vinywaji,
(xx) Stashahada ya Usimamizi wa Chakula na Vinywaji,
(xxi) Stashahada ya Huduma na Uuzaji wa Chakula na Vinywaji,
(xxii) Stashahada ya Uzalishaji wa Chakula na Lishe ya Binadamu,
(xxiii) Stashahada ya Sayansi na Teknolojia ya Chakula,
(xxiv) Stashahada ya Uzalishaji na Huduma za Chakula na Vinywaji,

(xxv) Stashahada ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu,

(xxvi) Stashahada ya Misitu,

(xxvii) Stashahada ya Uvuvi Mkuu, na

(xxviii) Stashahada ya Kilimo kwa Ujumla.

### 6.3.5 Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)

(i) Usalama wa Mtandao na Uchunguzi wa Kidijitali,

(ii) Teknolojia ya Midia ya Picha na Uhuishaji,

(iii) Teknolojia ya Midia ya Picha na Filamu,

(iv) Stashahada ya Uhandisi wa Vifaa vya Kupimia, na

(v) Stashahada ya Uhandisi wa Elektroniki na Mawasiliano.

## 7.0 VIPENGELE NA VIWANGO VYA MKOPO

Waombaji wa mkopo watakaofaulu watapewa fedha kulingana na kiwango cha uhitaji kilichothibitishwa au kama itakavyoamuliwa na Bodi. Kiasi cha juu kabisa cha mkopo kitapangwa katika vipengele vya mkopo kwa utaratibu ufuatao:-

- Chakula na Malazi,
- Ada ya Mafunzo,
- Vitabu na Viandikwa,

- Mahitaji Maalum ya Fani,
- Gharama za Utafiti, na
- Mafunzo kwa Vitendo.

**Kumbuka:** HESLB haitoi mikopo kwa msingi wa asilimia, bali hutolewa kwa jumla (lump-sum) na jumla hiyo itagharimia baadhi au vyote kati ya vipengele vifuatavyo:

## 7.1 Chakula na Malazi

Kiwango cha juu kabisa kitakachopangwa ni **TZS 7,500.00** kwa siku wakati wa mafunzo chuoni kulingana na kalenda ya taasisi husika. Kiasi hiki kitalipwa moja kwa moja kwa mwanafunzi.

## 7.2 Ada ya Mafunzo

Kiwango cha juu kabisa kitakachopangwa ni **TZS 1,200,000.00** kwa mwaka na kitalipwa kwa taasisi husika kama itakavyoidhinishwa na Bodi.

## 7.3 Vitabu na Viandikwa

Kiwango cha juu kabisa kitakachopangwa ni **TZS 200,000.00** kwa mwaka kwa ajili ya matumizi ya vitabu na vifaa vya kuandikia.

## 7.4 Mahitaji Maalum ya Kitivo

Kiwango cha juu kabisa kitakachopangwa ni **TZS 300,000.00** kwa mwaka na kitalipwa moja kwa moja kwa mwanafunzi.